

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, pages 162-163.

KUSAMBAZA MBINU YAKO: A SAMPULI YA KIPAJI CHA MBINU

Mradi wa mbinu mpya (*New Tactics Project*) unashugulikia kusoma na kufundisha mbinu mpya. Hatutaki ufikirie juu ya kazi yako kwa upande wa mbinu na pia ujifunze mbinu mpya kutoka humu kitabuni, bali pia usambaze mbinu zako kwa wengine. Kusambaza mbinu yafaidisha wale walioanzisha mbinu (kwa kujenga ujuzi wao wa uongozi na kipaji) na pia wale ambao wanafundisha.

Mwongozo mfupi wa dakika 40 za kipaji ya mbinu zako unafwata. Tumia huu mwongozo kukusaidia kuchagua yale mambo yatakayo saidia kikundi chako kuelewa na kutekeleza mbinu yako.

Kwa Dakika moja

Tamka mbinu Yako.

Anza mafundisho yako kwa kueleza kwa ufupi mbinu yako. Kumbuka kulenga shabaha yako kwa mbinu yako wala sio kwa shida au tatizo au muktadha. Rudia maana ya mbinu kwa p.21 na usome “*The Need for New Tactics*” p.12 ili usiwe na wasi wasi wowote juu ya hili jambo -maana ya mbinu.

Pia fikiria njia sisitizi ya kueleza kikundi chako ni kwa nini hii mbinu ni ya kipekee, muhimu au ya kufana. Waweza kusema hadithi ama ulize swali litakalo chemsha bongo za wasikilizaji wako.

Dakika 5

Eleza Muktadha

Wataka wasikilizaji wako waelewe ni kwa nini hii mbinu ilitumika kwa hii hali yako. Wasaidie kuelewa kwa njia ifuatayo:

- Eleza mambo ya maingiano ya wakati huu au ya kale yaliyohitaji mwitikio, sana sana yale yatakayosaidia wengine kuelewa mbinu yako.
- Eleza utaratibu ambao huu mwitikio ulipangiliwa
- Eleza matokeo unayonua kwa kutumia hii mbinu i.e. shabaha na malengo
- Kwa ufupi, eleza mkakati uliotumiwa na vile mbinu hii yaambatana na huo mkakati
- Sio lazima uchukue mda mrefu kueleza haya maswala lakini kumbuka kuyaguzia.

Dakika 20

Eleza vile Mbinu Yatumika

Hii ndio kiini ya kipaji. Kumbuka unapatia wasikilizaji wako maarifa muhimu watakayohitaji kutekeleza mbinu yako katika hali zao.

Eleza moja kwa moja vile ulitekeleza hii mbinu. Tungependelea utumie kesi moja maalum kama mfano. Fikiria mwenzako anayetoka nchi nyingine atastahili kujua nini? Atanza vipi? Ni watu ngapi watajikusisha? Wanahitaji usaidizi gani? Wanahitaji rasilmali gani?

Kumbuka kueleza moja kwa moja!

Dakika 7

Rudia maendeleo ya hiyo mbinu

Ongea juu ya shabaha: Mbinu hii yatarajiwa kuathiri tabia, taasisi, sera au mtu gani? Kumbuka kuwa kwaweza kuwa na shabaha ya kwanza na pia shabaha ya mwisho.

Eleza matokeo yakini. Walioshughulikia hili swala wanaeleza vipi matokeo wanayotarajia na pia maathara? Tumia misemo au maneno ya wale walioshughulikia hili swala.

Dakika 7

Eleza mafunzo uliyopata na vile mbinu hii yaweza kutumika kwingine

Eleza mafunzo uliyopata ukitekeleza hii mbinu. Nini ilifanya kazi? Ni nini ungefanya tofauti? Ni mawaidha au mapendekezo gani ungepeana kwa wengine?

Kwa mazoea yako, ni mambo gani ungependa yawekwe maanani kabla ya kutekeleza hii mbinu? Kuna malemeo gani?

Kama unajua matumizi mengine ya mbinu hii, Kwa ufupi, eleza vile ilitekelezwa kitofauti na ni kwa nini.